

HOTUBA YA MSTAHIKI MEYA WA JIJI LA DAR ES SALAAM, MHE. ISAYA  
MWITA CHARLES KATIKA HAFLA YA KUFUNGUA KITUO CHA URITHI WA  
UBUNIFU MAJENGO NA UTALII KATIKA JIJI LA DAR ES SALAAM

TAREHE 30 JUNI, 2017

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa  
na Michezo, Mhe. Dkt. Harrison Mwakyembe (MB),**

**Balozi wa Umoja wa Nchi za Ulaya, Mhe. Roeland Van De Geer,**

**Waheshimiwa Madiwani wa Dar es Salaam,**

**Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam, Bibi Sipora Liana**

**Rais wa Jumuiya ya Wasanifu Majengo Tanzania, Architect Henry  
Mwoleka**

**Mkurugenzi Mkuu wa Kituo cha Urithi wa Ubunifu Majengo, Bibi  
Aida Mulokozi,**

**Wageni waalikwa,**

**Waandishi wa Habari,**

**Mabibi na Mabwana,**

Ninapenda kuchukua fursa hii, awali ya yote, kumshukuru, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mhe. Dkt. Harrison Mwakyembe (Mb) kwa kukubali ombi letu la kuwa mgeni rasmi katika hafla ya ufunguzi wa Kituo cha Urithi wa Ubunifu wa Majengo na Utalii.

Tukio hili ni mafanikio makubwa sana katika juhudi zinazofanywa na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam za kukuza utalii wa Jiji letu kwa kutangaza vivutio vya utalii vilivyopo Dar es Salaam, ambapo sasa jengo hili linakuwa ni miongoni mwa vivutio vikubwa na kituo kikuu cha utalii katika Jiji la Dar es Salaam.

## **Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Miji mingi ya Afrika kama vile Mombasa, Zanzibar na Cape Town husifika sana kwa shughuli za utalii wa majengo ya kale ambayo huvutia idadi kubwa ya watalii kwenye miji hiyo. Kwetu Dar es Salaam pia tuna kila sababu ya kukuza, kuhifadhi na kutangaza vivutio vyetu vya utalii yakiwemo majengo ya kihistoria.

Jiji la Dar es Salaam ni maarufu sana kisiasa, kiuchumi, kibiashara na pia ni kitovu cha miundombinu na kiunganishi cha mikoa mbalimbali ya Tanzania na nchi za jirani kama Kenya, Uganda, Zambia, Burundi na Kongo kwa kuwa na uwanja wa ndege wa kimataifa, bandari, reli na kituo kikubwa cha mabasi yaendendayo sehemu mbalimbali za nchi na kulifanya Jiji hili kuunganika na vivutio vikubwa vya utalii kama mji wa kihistoria wa Bagamoyo, magofu ya Kilwa, Mbuga za wanyama za Mikumi na Sadani pamoja na visiwa vya Zanzibar.

## **Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Tunapozungumzia vivutio vya utalii katika Jiji letu ni vema kuvitaja baadhi yake ili wananchi waweze kutambua utajiri mkubwa tulionao katika eneo hili na malengo ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ya kukuza, kuhifadhi, kutangaza vivutio vya utalii tulivyonavyo na kuvifanya kuwa vyanzo vikubwa vya mapato katika Jiji letu.

Vivutio hivyo ni maeneo ya kihistoria, uwanda wa maji na fukwe, misitu, visiwa, sehemu za kitamaduni, asili ya watu na ukarimu, ngoma na sanaa za mikono. Kwa kuzitambua fursa hizo, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam imeandaa mipango ya kukuza utalii kwa kulitoa jengo letu la Old Boma kuwa kutumika kama Kituo cha Urithi wa Ubunifu Majengo na Utalii, kuweka nembo maalumu katika baadhi ya majengo ya kihistoria, kutoa mafunzo kwa madereva wa teksi wanaotoa huduma katika maeneo yanayotembelewa na watalii, kuwa na mabasi maalumu ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kwa ajili ya kutoa huduma kwa watalii.

## **Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Mafanikio tuliyoyapata na mipango ya kukuza utalii tunayoendelea nayo ni matokeo makubwa ya ushirikiano wetu na wadau mbalimbali katika sekta hii. Kwa fursa hii ningependa kutoa shukrani za dhati kwa Umoja wa Nchi za Ulaya kwa kufadhili mradi huu wa Kituo cha Urithi wa Ubunifu Majengo na Utalii ambacho nimejulishwa kwamba kituo hicho cha uhifadhi wa majengo ya kihistoria ni cha kwanza kufadhiliwa na Umoja wa Nchini za Ulaya katika Afrika Mashariki. Huo ni msaada mkubwa na wakujivunia kwa wananchi wa Dar es Salaam.

Ninawashukuru sana Jumuiya ya Wasanifu Majengo Tanzania kwa kusimamia ukarabati wa jengo, kuongeza uelewa wa wananchi juu ya uhifadhi wa majengo ya kale na kuonesha nia ya kuendelea kushirikiana na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kuhifadhi majengo ya kihistoria na kukuza utalii.

Rai yangu kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa katika Jiji la Dar es Salaam, taasisi mbalimbali za Serikali, wadau mbalimbali katika sekta ya uhifadhi majengo na utalii pamoja na wananchi wote kwa ujumla ni kufanya jitihada za kuyatambua, kuyatunza na kuyatangaza majengo hayo ya kihistoria yasiweze kufutwa na kasi ya maendeleo ya ukuaji wa miji katika Jiji la Dar es Salaam.

**ASANTENI KWA KUNISIKILIZA**